

Uthibitisho wa Biashara Ndogo na Zinazomilikiwa na Makundi Maalum: Je, inafaa kwa Biashara yako?



Jumuiya ya Madola ya Massachusetts inawajibika katika mchakato wa ukuwadi wa haki, wenye uwazi na ushindani, unaohakikisha kwamba biashara ndogo na zinazomilikiwa na makundi maalum zinajumuishwa katika mfumo wa usambazaji wa Jumuiya ya Madola. Endelea kusoma ili uone ikiwa biashara yako inaweza kunufaika inapothibitishwa na Ofisi ya Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Makundi Maalum (SDO).

Uthibitisho una manufaa gani?

Uthibitisho wa SDO unapatikana bila malipo yoyote kwa biashara yako. Kampuni zitakazothibitishwa zitapokea mialiko ya mafunzo, hafla za utangamano na ushirikisho wa kibiaresha. Muhimu zaidi, uthibitisho utawezesha kampuni yako kushiriki katika mipango hii tatu ya Jumuiya ya Madola:

- **Mipango wa Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Makundi Maalum (SDP)** ulianzishwa ili kukuza utofauti, usawa na ujumuishaji wa huduma na bidhaa katika kandarasi za serikali kwa kuhakikisha ushiriki kamili wa biashara za watu wa makundi maalum. Angalia kisanduku kilichoko kulia ili uone orodha ya makundi yanayostahiki.
- **Mipango wa Ununuzi wa Biashara Ndogo (SBPP)** unalenga kuhamasisha ukuaji wa biashara ndogo za Massachusetts. Lengo kuu la mipango hii ni kuongeza fursa za biashara kwa biashara ndogo na zinazomilikiwa na watu wa makundi maalum.
- **Mipango ya Kusawazisha Upangaji (ya Jimbo na Manispaa)** ilianzishwa kutoa fursa kwa MBE, WBE, SDVOBE na VBE katika uchoraji na ujenzi wa majengo ya serikali na majengo yanayofadhiiliwa na serikali.

Nani anastahiki kuthibitishwa?

Ustahiki unategemea mwongozo wa kila kategoria ya uthibitisho. Kawaida, mmiliki/wamiliki (umilikiwa asilimia 51) wa kampuni inayotuma ombi la uthibitisho sharti awe mshiriki wa kundi lillobainishwa— kwa mfano awe mwanamke, mwanachama wa kikundi cha wachache, au mkongwe. Mmiliki/wamiliki lazima wadumishe usimamizi wa kampuni kama kampuni huru na inayoendelea. Uthibitisho wa biashara ndogo za Massachusetts unategemea eneo la biashara, ukubwa na idadi ya wafanyakazi.

Kuthibitishwa na Ofisi Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Makundi Maalum

1. **Tembelea www.mass.gov/sdo/start** ili kujua ni thibitisho gani huenda zikafaa biashara yako na hatua unazopaswa kuchukua.
2. **Sajili biashara yako katika COMMBUYS.** Jiandikishe kupokea taarifa za zabuni mpya na ujifunze mengi kuhusu kandarasi za jimbo lote. Ikiwa biashara yako ndogo ipo Massachusetts, jiunge au usajili tena Ushiriki wako wa Mpango wa Ununuzi wa Biashara Ndogo.
3. **Ikiwa biashara yako ipo Massachusetts, hudhuria warsha ya kabla ya uthibitisho.** Pitia sheria na kanuni zinazohusu mchakato wa uthibitisho na mpango kusawazisha upangaji.
4. Biashara ambazo haziko Massachusetts, tafadhali tembelea ukurasa wa SDO wa “Certification Programs” www.mass.gov/sdo.
5. **Tuma ombi la uthibitisho** Kusanya hati zako na uwasilishe ombi lako ili lishughulikiwe.
6. **Anza kazi!** Uthibitisho ni mwanzo tu— tafiti wateja watarajiwa, jifunze zaidi kuhusu kandarasi, na uanze kujikuza kama biashara maalum.

Wasiliana Nasi! Kwa maelezo zaidi kuhusu uthibitisho wa biashara ndogo na maalum, mipango, sera, na fomu, tafadhali angalia tovuti ya SDO kwenye mass.gov/sd. Kwa maswali mengine, tutumie barua pepe kwa Webmaster.SDO@mass.gov.

Ofisi ya Biashara Zinazomilikiwa na Watu wa Makundi Maalum | One Ashburton Place, Room 1017 | Boston, MA 02108 | 617-502-8843

¹ PBE zinathibitishwa kwa ujumuishaji mdogo katika mipango anuwi za biashara maalum ilivyoelezwa kwenye 425 CMR §2.02.

Ilisasishwa Mei 2021